TANGAZO LA SERIKALI NA. 65 la tarehe 17/2/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI,

(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA MIPANGO MIJI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA KATIKA ENEO LA IKONDA YA MWAKA, 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mipango Miji ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Ikonda ya mwaka, 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililobainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina katika eneo la kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete.

*Tangazo la seriakali na (linaendelea)*

---

JEDWALI

---

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatavyo:-

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba IK1 yenye majira - nukta 635483MS, 8964423KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa $17^0$ kwa umbali wa kilomita 1.165 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba IK2 yenye majira - nukta 635140MS, 8965537KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa $73^0$ kwa umbali wa kilomita 0.946 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba IK3 yenye majira - nukta 634230MS, 8965799KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa $01^0$ kwa umbali wa kilomita 1.004 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba IK4 yenye majira - nukta 634208MS, 8964795KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa $58^0$ kwa umbali wa kilomita 0.940 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba IK5 yenye majira - nukta 635011MS, 8964306KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa $76^0$ kwa umbali wa kilomita 0.486 hadi ilipoanzia".

Dodoma,
.........., 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*